

شَهْرُ شَوَّالٍ

وَمَا يَتَعَلَّقُ بِهِ مِنَ الْأَحْكَامِ

MWEZI WA SHAWWAAL NA HUKUMU ZINAZOHUSIANA NAO⁽¹⁾

Mwandishi:

Abu Halima Arafat

¹- Makala hii ni ziada ya ile Makala yetu kuhusiana saumu ya siku sita katika mwezi wa Shawwaal, tuliyoandika 3/Shawwaal/1445^H – 12/4/2024^M. Alhamdulillah, ndani yake kuna faida nyingi ambazo hatukuzitaja kwenye Makala iliyopita, kadhaalika kuna marekebisha kama katika baadhi sehemu, kama utakavyoona hilo ndugu msomaji.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

FADHILA ZA KUFUNGA SIKU SITA ZA MWEZI WA SHAWWAAL:

Imepokewa kutoka kwa Abu Ayoub Al Answariy رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ kwamba Mtume صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ amesema:

«مَنْ صَامَ رَمَضَانَ، ثُمَّ أَتْبَعَهُ سِتًّا مِنْ شَوَّالٍ، كَانَ كَصِيَامِ الدَّهْرِ»

“Mwenye kufunga Ramadhani kisha akafuatishia siku sita za (mwezi wa) Shawwaal, ni sawa na kufunga mwaka mzima”. Muslim (204), Abu Daud (2433).

Amesema Imam Nnawawi-Allaah amrehemu-:

"يُسْتَحَبُّ صَوْمُ سِتَّةِ أَيَّامٍ مِنْ شَوَّالٍ لِهَذَا الْحَدِيثِ"

“Kwa Hadithi hii inapendekezwa kufunga siku sita za mwezi wa Shawwaal”⁽²⁾.

Amesema Ibn Muflih -Allaah amrehemu-:

"وَيُسْتَحَبُّ إِتْبَاعُ رَمَضَانَ بِسِتِّ مِنْ شَوَّالٍ"

“Inapendekezwa kufuatishia Ramadhani kwa kufunga siku sita za Shawwaal”⁽³⁾.

Kadhalika jopo la Maulamaa wa Al Lajnat Ad Daaima wamesema:

“فَهَذَا حَدِيثٌ صَحِيحٌ يَدُلُّ عَلَى أَنَّ صِيَامَ سِتَّةِ أَيَّامٍ مِنْ شَوَّالٍ سُنَّةٌ، وَقَدْ عَمِلَ بِهِ الشَّافِعِيُّ وَأَحْمَدُ وَجَمَاعَةٌ مِنْ أُمَّةٍ مِنَ الْعُلَمَاءِ”

“Hii ni hadithi sahihi inayofahamisha kwamba kufunga siku sita za mwezi wa Shawwaal ni Sunnah, na Imamu Al-Shafi’, Ahmad na kundi kubwa la Maimamu miongoni mwa Maulamaa wameifanyia kazi hadithi hii”. (Jz. 10, Uk. 390).

Je, saumu ya sita inamhusu mwanaume na mwanamke?

Amesema Ibn Uthaymin-Allaah amrehemu-:

"وَهُوَ عَامٌّ لِلرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ"

“Nayo inamuenea mwanaume na mwanamke”. Al Majmu: (Jz. 17, Uk. 20).

²- Al Majmuu’ (Jz. 6, Uk. 227).

³- Al Furuu’ (Jz. 5, Uk. 84).

Je, atafunga sita mtu anayedaiwa baadhi ya masiku ya Ramadhani?

Amesema Ibn Uthaymin-Allaah amrehemu-:

"صِيَامُ سِتَّةِ أَيَّامٍ مِنْ شَوَّالٍ لَا يَحْصُلُ ثَوَابُهَا إِلَّا إِذَا كَانَ الْإِنْسَانُ قَدِ اسْتَكْمَلَ صِيَامَ شَهْرِ رَمَضَانَ"
"Saumu ya siku sita za Shawwaal, hayapatikani malipo yake isipokuwa kwa mtu ambaye amekamilisha kufunga mwezi wote wa Ramadhani"⁽⁴⁾.

Na amesema sheikh Ibn Baaz-Allaah amrehemu-:

"فَالْوَجِبُ الْمُبَادَرَةُ بِالْقَضَاءِ، وَلَوْ فَاتَتْ السِّتَّةُ... وَلِأَنَّ الْفَرَضَ مُقَدَّمٌ عَلَى النَّفْلِ"
"Wajibu ni kufanya haraka kulipa (deni la ramadhani), hata kama zitampita siku sita... na kwa sababu faradhi inatangulizwa kuliko Sunnah"⁽⁵⁾.

Amesema Ibn Rajab Al Hambaliy-Allaah amrehemu-:

"فَمَنْ كَانَ عَلَيْهِ قِضَاءٌ مِنْ رَمَضَانَ ثُمَّ بَدَأَ بِصِيَامِ سِتِّ مِنْ شَوَّالٍ... لَمْ يَحْصُلْ لَهُ ثَوَابٌ مِنْ صَامِ رَمَضَانَ ثُمَّ اتَّبَعَهُ بِسِتِّ مِنْ شَوَّالٍ... لِأَنَّ صِيَامَ السِّتِّ مِنْ شَوَّالٍ إِنَّمَا تَكُونُ بَعْدَ إِكْمَالِ عِدَّةِ رَمَضَانَ."
"Yule ambaye ataanza kufunga siku sita za Shawwaal hali ya kuwa inampasa yeye kulipa masiku anayodaiwa katika Ramadhani... hatopata yeye malipo ya yule aliyefunga Ramadhani kisha akafuatishia siku sita za mwezi wa Shawwaal...kwa sababu kufunga siku sita za Shawwaal hupatikana baada ya kukamilisha idadi ya siku za Ramadhani"⁽⁶⁾.

Je, ni lazima afunge siku sita za mwanzo wa mwezi wa Shawwaal?

Amesema sheikh Ibn Baaz-Allaah amrehemu-:

"يَخْتَارُهَا الْمُؤْمِنُ مِنْ جَمِيعِ الشَّهْرِ، فَإِذَا شَاءَ صَامَهَا فِي أَوَّلِهِ، أَوْ فِي أَثْنَانِهِ، أَوْ فِي آخِرِهِ"
"Muislamu ana khiyari katika mwezi wote wa Shawwaal, akitaka atazifunga siku sita mwanzo wa mwezi, au katikati, au mwisho wa mwezi"⁽⁷⁾.

⁴- Majmuu al Fataawa (Jz. 18, Uk. 20).

⁵- Majmuu Fataawa Ibn Baaz (Jz. 15, Uk. 393).

⁶- Latwaaif al Ma'arif (Jz. 1, Uk. 223).

⁷- Majmuu Fataawa Ibn Baaz (Jz. 15, Uk. 390).

Ni ipi njia nzuri ya kufunga siku sita za Shawwaal?

Amesema Ibn Uthaymin-Allaah amrehemu-:

"الْأَفْضَلُ أَنْ يَكُونَ صِيَامُ سِتَّةِ أَيَّامٍ مِنْ شَوَّالٍ بَعْدَ الْعِيدِ مُبَاشَرَةً، وَأَنْ تَكُونَ مُتَتَابِعَةً"

“Iliyo bora ni kufunga siku sita za Shawwaal baada tu ya siku ya Eid, na zifuatane”. Majmuu al Fataawa (Jz. 20, Uk. 20).

Je, ni wajibu kufunga siku sita za Shawaal kila mwaka?

Amesema Ibn Uthaymin-Allaah amrehemu-:

"إِذَا صَامَهَا بَعْضَ السِّنِّينَ وَتَرَكَهَا بَعْضَ السِّنِّينَ فَلَا بَأْسَ، لِأَنَّهَا تَطَوُّعٌ وَلَيْسَتْ فَرِيضَةً"

“Akifunga baadhi ya miaka na miaka mingine akaacha hapana vibaya, kwa sababu kufunga hizo (sita) ni Sunnah si wajibu”. Al Majmuu: (Jz. 20, Uk. 21).

Je, hadithi ya kufunga siku sita za Shawwaal ni dhaifu?

amesema Ibnul Qayyim -Allaah amrehemu- wakati anataja sababu zinazotajwa kuikataa hadithi ya kufunga sita, akasema:

"وَهَذِهِ الْعِلَلُ - وَإِنْ مَنَعْتَهُ أَنْ يَكُونَ فِي أَعْلَى دَرَجَاتِ الصَّحِيحِ - فَإِنَّهَا لَا تُوجِبُ وَهَنَهُ"

“Na kasoro hizi, hata kama zitazuia hadithi hiyo kuwa katika viwango vya juu vya usahihi, lakini hazipelekei kuifanya kuwa dhaifu”⁽⁸⁾.

Kadhaalika Al Mubaarakfuuriy-Allaah amrehemu-:

"قَوْلُ مَنْ قَالَ بِكَرَاهَةِ صَوْمِ هَذِهِ السِّتَّةِ بَاطِلٌ مُخَالَفٌ لِأَحَادِيثِ الْبَابِ"

“Kauli ya yule anayeona ni karaha kufunga siku hizi sita, (hiyo) ni kauli batili inapingana na hadithi nyingi zilizokuja kwenye mlango huu”⁽⁹⁾.

Ni Sunnah kuoa au kuoza katika mwezi wa Shawwaal:

Amesema Aisha-Allaah amridhie-:

"تَزَوَّجَنِي رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي شَوَّالٍ، وَأَدْخَلْتُ عَلَيْهِ فِي شَوَّالٍ"

“Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alinioa mimi katika mwezi wa Shawwaal na aliniingilia katika mwezi wa Shawwaal”. Musnad Ahmad (24272).

⁸- Tahdhiibu Sunan Abi Daud (Jz. 1, Uk. 476).

⁹- Tuhafatul Ahwadhi (Jz. 3, Uk. 389)

Amesema Imam An Nawawi-Allaah amrehemu-:

"فِيهِ اسْتِحْبَابُ التَّزْوِيجِ وَالتَّزْوُجِ وَالدُّخُولِ فِي شَوَّالٍ"

“Kuna katika hadithi hii Sunnah ya kuzoesha, kuoa na kuanza kufanya jimai (na mke mpya) katika mwezi wa Shawwaal”⁽¹⁰⁾.

Katika wakati wa Jaahiliyyah (kabla ya Uislamu), waarabu walikuwa na itikadi kwamba kuoa katika mwezi wa Shawwaal ndoa inakosa furaha na mapenzi, lakini -Alhamdulillah- Uislamu umeivunja itikadi hiyo, kama vile ulivyovunja itikadi ya baadhi wajinga wanaodhani kwamba haifai kuoa wala kufanya jimai na bibi harusi siku ya Eid al-Fitr na Eid al-Adh-ha

Amesema Ibn Kathir -Allaah amrehemu-:

"وَفِي دُخُولِهِ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ بِهَا فِي شَوَّالٍ، رَدُّ لِمَا يَتَوَهَّمُهُ بَعْضُ النَّاسِ مِنْ كَرَاهِيَةِ الدُّخُولِ بَيْنَ الْعِيدَيْنِ خَشْيَةَ الْمَفَارَقَةِ بَيْنَ الزَّوْجَيْنِ، وَهَذَا لَيْسَ بِشَيْءٍ"

“Na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kumwingilia kwake Aisha -Allaah amridhie- katika mwezi wa Shawwaal, ni majibu kwa kile ambacho baadhi ya watu wanadhania, nacho ni kuchukia mtu kumwingilia (mke wake) katika siku ya Eid mbili kwa ajili ya kuhofia kuwatenganisha wanandoa, lakini hili si kweli”⁽¹¹⁾

Hadithi hii ni Maudhu’ (uwongo):

"مَنْ صَامَ رَمَضَانَ، وَاتَّبَعَهُ سِتًّا مِنْ شَوَّالٍ؛ خَرَجَ مِنْ ذُنُوبِهِ كَيَوْمِ وَلَدَتْهُ أُمُّهُ"

“Mwenye kufunga Ramadhani na akafuatishia siku sita za Shawwaal, anaepukana na madhambi yake (na anakuwa) kama siku aliyozaliwa na mama yake”⁽¹²⁾.

Hadithi hii ni dhaifu:

"مَنْ صَامَ رَمَضَانَ وَسِتًّا مِنْ شَوَّالٍ وَالْأَرْبَعَاءَ وَالْخَمِيسَ دَخَلَ الْجَنَّةَ"

“Mwenye kufunga Ramadhani na siku sita za Shawwaal, na jumatano na al khamis, ataingia peponi”. [Dha’if al Jaami’ (5650)].

¹⁰- Sharh An Nawawi ala Muslim (Jz. 9, Uk. 209).

¹¹- Al Bidaayat Wan Nihaayat (Jz. 4, Uk. 570-571).

¹²- Ad Dhaai’fa (5190).

Bidaa inayofanywa katika Ijumaa ya mwisho ya Ramadhani:

Kuna bidaa nyingi zinafanywa na baadhi ya Masufi katika Ijumaa ya mwisho ya ramadhani, ikiwemo kuswali raka nne kwa madai ya kwamba ni kafara ya swala zote zilizompti mtu katika Maisha yake!

Amesema sheikh Ibn Uthaymin-Allaah amrehemu- wakati akijibu swali aliloulizwa kuhusiana na swala hii:

"الْحُكْمُ فِي هَذِهِ الصَّلَاةِ أَنَّهَا مِنَ الْبِدَعِ، وَلَيْسَ لَهَا أَصْلٌ فِي الشَّرِيعَةِ الْإِسْلَامِيَّةِ، وَهِيَ لَا تَزِيدُ الْإِنْسَانَ مِنْ رَبِّهِ إِلَّا بُعْدًا"

"Hukumu ya swala hii ni bidaa, haina asili yoyote katika sheria ya Kiislamu, na swala hii hamzidishii mtu isipokuwa kumuweka mbali na Allaah"⁽¹³⁾.

Bidaa inayofanyika siku ya tarehe 8 Shawwaal "Eidul Abraar":

Amesema Ibn Taymiyyah -Allaah amrehemu-:

"وَأَوْثَانٌ مِنْ سُؤَالِ الَّذِي يُسَمِّيهِ الْجُهَّالُ عِيدَ الْأَبْرَارِ، فَإِنَّهَا مِنَ الْبِدَعِ الَّتِي لَمْ يَسْتَحِبَّهَا السَّلَفُ وَلَمْ يَفْعَلُوهَا"
"Au tarehe 8 shawwaal ambayo wajinga wanaiita Sikukuu ya watu wema, hiyo ni miongoni mwa bidaa, wala Salaf hawakuipendekeza wala hawakuifanya"⁽¹⁴⁾.

Amesema Ibn Taymiyyah-Allaah amrehemu-:

"وَأَمَّا تَأْمِينُ سُؤَالِ فَلَيْسَ عِيدًا لَا لِلْأَبْرَارِ وَلَا لِلْفُجَّارِ وَلَا يَجُوزُ لِأَحَدٍ أَنْ يَعْتَقِدَهُ عِيدًا وَلَا يُحَدِّثَ فِيهِ شَيْئًا مِنْ شَعَائِرِ الْأَعْيَادِ"

"Na tarehe nane ya Shawwaal si Eid (sikukuu) ya watu wema wala waovu, wala haifai kwa mtu yeyote kuitakidi siku hiyo kuwa ni sikukuu, wala asizushe katika siku hiyo jambo lolote katika alama za Eid (sikukuu)"⁽¹⁵⁾.

Namuomba Allaah aniruzuku Taufiq na Qabul

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud
Ijumaa 10/Shawwaal/1445^h - 19/4/2024^m.**

¹³- Majmuu al Fataawa (Jz. 12, Uk. 188).

¹⁴- Al Fataawal Kubra (Jz. 4, Uk. 414)].

¹⁵- Al Fataawal Kubra (Jz. 5, Uk. 379)].